# TINGATINGA WASAKA TONGE CLUB:

**(TWTC)**

# KATIBA YA KLABU:

# UTANGULIZI:

- Ni kikundi cha hiari chenye lengo la kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuinua wanachama wake kiuchumi.
- Kikundi hiki kimeanzishwa rasmi tarehe **16.03.2025** Kwa pamoja wanachama wanaahidi kuilinda na kuitekeleza katiba hii.
- Pamoja na Katiba hii, Kikundi hiki kitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni mbalimbali ambazo zitawekwa na wanachama.

# SURA YA KWANZA:

### JINA, ANUANI NA TAFSIRI.

**1.0. JINA LA KLABU**

Kikundi hiki kitajulikana kwa jina la **TINGA TINGA WASAKA TONGE CLUB (TWTC)** Makao makuu ya Klabu hii yatakuwa Kijiji cha Tinga Tinga, Kata ya Tinga Tinga, Tarafa ya Enduimet, Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha Tanzania.

Anuani ya klabu hiki itakuwa ni
**TINGA TINGA WASAKA TONGE KLAB,**
**S.L.P ---------,**
**LONGIDO – ARUSHA ,**
**TANZANIA.**
**E-mail:** wasakatongemoneyclub@yahoo.com
**Hotline: +255 766 297 062:**

**1.1 TAFSIRI**

Kwa mujibu wa Katiba hii, maneno yafuatayo yatakuwa na maana ifuatayo;

i) Mwanachama: Mtu yeyote atakayekidhi vigezo vya kuwa mwanachama

ii) Mwanachama hai : Mwanachama anayetimiza masharti ya kuwa mwanachama kwa mujibu wa katiba hii.

iii) Kanuni: Muongozo wa jinsi ya uendendeshaji wa klabu

iv) Kikundi au Klab: Taasisi hii inayoanzishwa kwa mujibu wa katiba ambayo inatambulika kama TINGA TINGA WASAKA TONGE CLUB

v) Tatatizo: Ina maana ya changamoto kwa mujibu wa katiba hii.

vi) Utovu wa Nidhamu: Kitendo chochote kile kinacho kinzana na Katiba hii pamoja na kanuni zake.

vii) Hisa; Ni thamani ya kiwango cha fedha zinazowekwa katika mfuko wa pamoja.

# SURA YA PILI:

**2.0 AINA YA KLABU**

WASAKA TONGE CLUB ni Kikundi cha Kijamii cha Kimaendeleo ya Kiuchumi (Community Based Organisation/CBO)

**2.1 MADHUMUNI NA MALENGO YA KLABU.**

Kikundi hiki kipo kwa kutimiza au kutekeleza yafuatayo..

i) Kushirikiana kufanya miradi mbalimbali ya Kiuchumi na Kijamii kwa maendeleo ya kikundi na ustawi wa wanachama

ii) Kuanzisha mfuko wa kikundi wa kukopa na kuwekeza hisa.

iii) Kushirikiana na kusaidiana nyakati za shida na raha.

iv) Wanakikundi kuwezeshana katika kuimarisha hali zao za Kipato ili kuweza kuwa na maisha yaliyo bora zaidi.

**2.2 MALENGO YA KLABU.**

Ili kuweza kufikia matarajio ya Kikundi kitafanya yafuatayo:-

(i) Kuweka utaratibu mahsusi wa kununua HISA kila wiki kwa wanachama ikiwa ndio msingi wa chanzo cha mapato.

(ii) Kubuni Miradi mbalimbali itakayosimamiwa na kuendeshwa na wanachama wenyewe au hata kwa msaada wa kiufundi kutoka nje ya kikundi.

(iii) Kuandaa maandiko ya kuwezesha miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa wanachama kutoka kwa serikali, washirika wa ndani na nje ya Tanzania.

(iv) Kuimarisha Ushirikiano na wanachama wenye changamoto mbalimbali kama vile; Maradhi, Misiba, Harusi, Sherehe, Majanga ya Kiasili na matukio mengine yanayolingana na hayo.

# SURA YA TATU:

**3.0. UANACHAMA.**

Kutakuwa na aina mbili zifuatazo za uanachama ambazo ni;

**3.1.1 Mwanachama wa Kawaida.**

Ni mtu yeyote yule ambaye ametimiza taratibu zote za kujiunga na Kikundi au Umoja huu kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kulipa Ada na Michango stahiki.

**3.1.2 Mwanachama wa Kutunukiwa.**

Mwanachama wa Kutunukiwa ni Mtu yeyote atakaetunukiwa uanachama kupitia maamuzi au azimio la Mkutano Mkuu katika kuthamini Mchango uliotolewa na Mtu huyo ama atakaoendelea kuutoa kwa kuleta maendeleo na ufanisi wa Malengo ya Kikundi au Umoja huu.

**3.2. SIFA ZA MWANACHAMA.**

i) Awe na Umri usiopungua miaka 18.

ii) Awe mwenye nia na awe tayari kuwa mwanachama.

iii) Awe tayari kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kikundi

iv) Awe na akili timamu.

v) Awe tayari kutii na kufuata masharti ambayo yameainishwa kwenye Katiba na Kanuni za kikundi

vi) Awe tayari kulipa kiingilio pamoja na ada ya uanachama ya kila mwezi.

vii) Awe kijana wa ndani ya Kijiji Cha tinga tinga.

### 3.3. HAKI ZA MWANACHAMA.

i) Kutoa maoni yake kwa uhuru

ii) Kuchagua au kuchaguliwa katika nafasi yoyote ile ya Uongozi katika Kikundi au Umoja huu.

iii) Kuwasiliana na Uongozi/Viongozi ikiwa ni pamoja na kupokea na kutoa taarifa zinazohusu Kikundi au Umoja huu.

iv) Kuhudhuria na/au kuwakilisha katika jambo lolote lile linalohusu Kikundi au Umoja huu kwa kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba hii.

v) Kupewa nafasi ya kujieleza na kujitetea pindi anapokabiliwa na tuhuma zozote zile dhidi yake katika umoja huu.

vi) Kutumia Mali za Kikundi kwa kufuata utaratibu na Kanuni za Umoja huu.

vii) Ana haki ya kutoa hoja yake na kusikilizwa wakati wa kushiriki majadiliano kwenye vikao.

viii) Kufahamu mapato na matumizi ya Kikundi kwa kutumia na kuzingatia Kanuni.

ix) Kusaidiwa linapomtokea tatizo.

x) Kusaidiwa kimawazo au kiuchumi kulingana na hali itakavyo ruhusu.

## 3.4. WAJIBU WA MWANACHAMA.

i) Kuilinda na kuitetea katiba hii wakati wote.

ii) Kutekeleza majukumu atakayopewa na viongozi au wanachama wenzake.

iii) Kushiriki katika shughuli zote za kikundi kwa mujibu wa katiba hii ikiwa ni pamoja na vikao halali vya Umoja huu.

iv) Kulipa ada pamoja na michango mbalimbali itakayo pitishwa na Kikundi au Umoja huu.

v) Kueneza sifa nzuri za Umoja huu.

vi) Kutii na kufuata maagizo na maazimio ya Mkutano/Mikutano halali ya Umoja huu, hata ikiwa hatakuwepo kwenye Mkutano huo, au hakushiriki katika kupitisha azimio hilo.

vii) Kuwa na nidhamu wakati wa Mikutano ama shuhuli nyingine zozote za Kikundi.

viii) Kutunza siri zote za Umoja huu

## 3.5. KUJIUNGA AU KUJIONDOA KWENYE KLABU.

### 3.5.1 KUJIUNGA NA KLABU.

**a)** Kujaza Fomu ya maombi itakayotolewa kwa ada itakayokuwa imepangwa.Maombi haya ni lazima yapitiwe na kukubaliwa na Uongozi, kisha kupitishwa na Mkutano Mkuu au Mkutano Mkuu Maalum.
Ada ya kuchukua fomu ni kiasi cha Tsh **10,000.00**

**b)** Baada ya kukubaliwa Mwombaji atatakiwa kulipa Ada ya kiingilio cha kiasi kitakachokuwa kimepangwa na Mkutano Mkuu au Mkutano Mkuu Maalum kwa wakati huo.
Kiingilio cha kujiunga na kikundi ni kiasi cha Tsh **50,000.00**

**c)** Pamoja na Ada ya kuchukua fomu na kiingilio Mwanachama mpya ni lazima kununua hisa yenye thamani ya Miezi Miwili Ili aweze kukamilisha usahili na kupata kadi ya uanachama pamoja na namba ya malipo kwa manunuzi ya hisa.

### 3.5.2 KUJIONDOA KWENYE KLABU.

***a)*** Kuchukua na kujaza fomu ya maombi ya kujiondoa katika klabu.
***b)*** Gharama za kujiunga, ada ya kuchukua fomu, michango na faini hazitarejeshwa kutoka katika klabu**.**
***c)*** Kurejesha mali zote za klabu mfano Kadi ya uanachama, kofia, tisheti au mali yoyote ya klabu.
***d)*** Kukatwa 7-8% ya hisa zake alizonunua.
***e)*** Mwanachama mwanzilishi atakapojitoa katika klabu na kutaka kurejea kuwa mwanachama atafata taratibu zote za kujiunga na klabu kisa kusubiri kwa muda wa miezi 3-6 ndipo kuandika barua ya maombi kurejeshewa uanachama.

## 3.6 MICHANGO

### 3.6.1 ADA YA UANACHAMA

- Kila Mwanachama ni lazima kulipa ada ya Uanachama kiasi cha **Tsh 5,000.00** kama ilivyoainishwa katika Sura ya 8 kipengele kidogo cha (ii) ya Katiba hii.

**ILI MRADI IELEWEKE KWAMBA;**

- Mwanachama ambaye alikuwa na taarifa juu ya uanzishwaji wa kikundi na hakujiunga wakati huo, endapo atataka kujiunga baadae, atatakiwa kulipa kiingilio na michango yote tangu kikundi kilipoanza mpaka kilipofikia, ndipo ataweza kukubaliwa kuwa mwanachama.

### 3.6.2 MICHANGO MINGINEYO.

- Kila Mwanachama atawajibika kuwasilisha mchango mwingine wowote ule utakaoamuliwa kuchangishwa kwa azma ya kukidhi miongoni mwa matarajio ya Umoja huu kama yalivyoainishwa katika sura ya 2 kipengele cha (iv) ya Katiba hii na kima kitakachokuwa kimeamuliwa.

### 3.6.3 MICHANGO YA HIARI

- Kutakuwa na michango ya hiari ambayo mtu hatolazimishwa bali anaweza kujitolea mali au fedha kwa mapenzi yake mwenyewe kwa lengo la kukijenga na kuendeleza klabu.

### 3.7. KUKOMA UANACHAMA.

Mwanachama anaweza kukoma kuwa mwanachama katika mazingira yafuatayo:-

i) Kujitoa kwa hiari yake mwenyewe kwa kufuata utaratibu kama ulivyo ainishwa katika sura ya 3.5.2

ii) Kushindwa kulipia ada ya kila mwezi kwa miezi mitatu mfululizo bila sababu yoyote ya msingi na kupoteza haki zake za kikatiba.

iii) Kutohudhuria vikao vitatu mfululizo vilivyowekwa kwa mujibu wa katiba hii bila taarifa na kupoteza haki zake za kikatiba.

iv) Kupuuza taarifa zinazotaka ushiriki wake katika shughuli za wanachama.

v) Kupoteza sifa kutokana kwa utovu mambo ya nidhamu.

vi) Ikiwa mwanachama atafariki.

vii) Kushidwa kununua hisa za kila wiki, kwa muda wiki kumi na mbili mfululizo hivyo atapoteza haki zote.

**ILI MRADI IELEWEKE KWAMBA,**

- Mtu aliyeacha au kufukuzwa Uanachama(uanakikundi) anaweza kuomba kujiunga tena na klabu baada ya miezi 6 kwa kufuata utaratibu wa kujiunga na Klabu kama inavyoonyesha katika sura ya 3.5.1

- Kama mwanachama atakoma kutokana na vigezo tajwa hapo juu, atakuwa amepoteza haki zake zote za msingi kama mwanachama.

# SURA YA NNE:

**4.0 UONGOZI.**

**4.1 Kikundi hiki kitakuwa na viongozi wafuatao:-**

i) Mwenyekiti

ii) Katibu

iii) Mweka Hazina

**4.2 KAMATI ZA KLABU.**

**4.2. i Kamati ya Utendaji.**

Itakayoundwa na wajumbe wafuatao:-

1. Mwenyekiti
2. Katibu
3. Mweka Hazina
4. Wajumbe wawili watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu.

**4.2. i. Kazi ya Kamati Tendaji.**

i) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya vikao halali vya Kikundi au Umoja huu.

ii) Kukutana wakati wa dharura na kujadili suala lilipo mbele yao na kulitolea uamuzi kwa niaba ya wanachama wote.

iii) Kuandaa agenda za mkutano mkuu.

iv) Kuandaa taarifa mbalimbali kwenye mkutano mkuu.

v) Kasimamia shughuli zote za kimaendeleo na ukuaji wa taasisi

vi) Kujadili na kuyafanyia kazi mambo mbali mbali yanayohusu wanachama au klabu kwa ujumla wake.

**4.2. ii. Kamati ya Mipango na Fedha.**

Kamati hii itaundwa na wajumbe watano watakao teuliwa na mkutano mkuu wa kikundi.

i) Mweka Hazina
ii) Mjumbe
iii) Mjumbe
iv) Mjumbe
v) Mjumbe

Wajumbe wa kamati hii watachagua kutoka mingoni mwao na kumpata Mwenyekiti na Katibu siku ya kikao cha kwanza cha kamati hii.

**4.2.ii Kazi za Kamati ya Fedha na Mipango.**

i) Itakayokuwa na kazi ya kubuni, kushauri na kuelekeza juu ya miradi yote ya kimaendeleo ya kikundi hiki.

ii) Itakuwa na kazi ya kusimamia utekelezaji wa miradi na mambo yote ya fedha ya kikundi

iii) Kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi ya fedha na mali za kikundi kwa kufuata Kanuni zilizowekwa.

**4.2.iii Kamati ya Sheria na Nidhamu**

i) Kamati hii itakuwa na jukumu la kusimamia nidhamu na kushughulikia migogoro baina ya wanachama, Lakini pia kutatua migogoro baina ya klabu na jamii. Kamati hii itaundwa na wajumbe watatu watakaoteuliwa na wanachama.

ii) Mwenyekiti wake kama itawezekana awe ni mtu mwenye elimu ama ufahamu wa sheria na taratibu za nchi na kimataifa pia.

iii) Kama hatakuwepo mtu wa kukidhi kigezo hicho, mtu mwingine yeyote mwenye busara , nidhamu na sifa ya usuluhishi atateuliwa na wanakamati wenyewe kuwa Mwenyekiti.

# SURA YA TANO:

**5.0 KAZI ZA VIONGOZI.**

**5.1. Majukumu ya Mwenyekiti.**

i) Atakuwa msemaji mkuu wa klabu.

ii) Ataitisha mikutano yote ya klabu.

iii) Ataitisha mkutano wa dharura pale itakapokuwa inahitajika.

iv) Ataongoza mikutano yote ya wanachama wote.

v) Atakuwa ndio Kiongozi Mkuu wa Klabu au Umoja huu.

**5.2 Majukumu ya Katibu.**

i) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa klabu.

ii) Kuandaa ajenda za vikao vyote.

iii) Ataandika kumbukumbu za vikao vyote vya klabu.

iv) Atakuwa anatoa taarifa ya maendeleo ya klabu mara moja kwa mwezi

v) Kwa kushirikiana na Mwenyekiti atakuwa anaandaa yatokanayo na vikao vilivyopita

vi) Atakuwa mtunza kumbukumbu na nyaraka mbalimbali za klabu.

vii) Atakuwa katibu wa kamati ya utendaji.

viii) Atakuwa mjumbe wa kamati ya Fedha na Mipango.

ix) Atawajulisha wanachama taarifa zote za vikao.

x) Atafanya kazi zote kadri atakavyoelekezwa na Mwenyekiti

## 5.3 Majukumu ya Mweka Hazina.

i) Atakuwa mtunza fedha za klabu.

ii) Atakusanya / atapokea fedha zote za kikundi na kutoa stakabadhi.

iii) Atakuwa mtunza nyaraka zote zinazohusiana na masuala ya fedha.

iv) Atatoa taarifa ya mapato na matumizi ya kikundi kila miezi mitatu.

v) Atafanya malipo yote halali ya klabu.

vi) Atajibu hoja zote zinazo husiana na masuala ya fedha.

vii) Atakuwa mjumbe wa kamati ya utendaji pamoja na kamati ya Fedha na Mipango.

# SURA YA SITA:

**6.0. VIKAO**

Kikundi hiki kitaongozwa kwa kufanya vikao mbali mbali kama vifuatavyo.

**6.1 Mkutano Mkuu**

- Klabu itakuwa na mkutano mkuu utakaofanyika mara moja kwa mwaka kwa kukutana ana kwa ana. Ili mkutano huu ufanyike idadi ya wajumbe watakohudhuria kikao hicho ni lazima iwe siyo chini ya asililimia HAMSINI (50%) ya wajumbe wote walio hai

**6.1. Kazi za Mkutano Mkuu.**

i) Kuchagua viongozi wa kikundi.

ii) Kupokea taarifa za mapato na matumizi kwa mwaka mzima.

iii) Kupokea taarifa ya kazi zote za mwaka.

iv) Kufanya mabadiliko au marekebisho kwenye vifungu mbalimbali vya katiba.

v) Kuidhinisha mipango ya kimaendeleo ya kikundi

vi) Kufanya Uchaguzi wa viongozi ikiwa muda umewadia.

**6.2.a Mkutano wa Kawaida wa Wanachama Wote.**

- Mkutano huu utafanyika mara moja kwa mwezi, kwa njia ya mtandao (whatsApp voice call au video call) siku na tarehe zitajulishwa na katibu wiki moja kabla.
- Ili mkutano huu ufanyike ni lazima idadi ya wajumbe ifikie asililimia 50% ya wajumbe wote walio hai.
- Endapo kikao kitasitishwa mara mbili kwa kukosa akidi, kikao cha tatu kitaendelea hata kama akidi itakuwa haijafikiwa na maamuzi ya kikao yatakuwa maamuzi halali ya kikundi.

**6.2. b. Kazi za Mkutano wa Kawaida wa Wanachama Wote.**

i) Kupokea taarifa ya utendaji na uendeshaji kikundi kwa mwezi husika.

ii) Kukusanya michango ya kila mwezi toka kwa wanachama.

iii) Kupata taarifa za utekelezaji wa maagizo na malengo yoyote ya kikundi.

iv) Kupokea taarifa ya fedha ya mwezi husika.

v) Kupitisha maamuzi ya kamati mbalimbali za kikundi.

vi) Kujadili na kulitolea uamuzi suala lolote litakalokuwa limejitokeza.

vii) Kupanga tarehe na sura ya kufanyia mkutano wa mwezi unaofuata.

**6.3 Kikao cha Kamati ya Utendaji.**

- Kutakuwa na vikao vya mara kwa mara vya kamati ya utendaji kadri itakavyohitajika ikiwa ni lazima kufanyika mara tatu kwa mwaka.
- Kazi za vikao hivi ni kama ilivyoonyeshwa kwenye kifungu cha 4.2.2 cha katiba. Ili vikao hivi vifanyike ni lazima idadi ya wajumbe wa kamati wafikie asililimia 50% ya wanakamati ya utendaji walio hai.

## 6.4. Kikao cha kamati ya Fedha na Mipango.

- Kamati hii itakua na vikao kadri itakavyohitajika kufanya hivyo ikiwa na vikao vitatu vya lazima kwa mwaka.
- li vikao hivi vifanyike ni lazima idadi ya wajumbe wa kamati wafikie asililimia 50% ya wanakamati wote walio hai.

## 6.5. Kazi za vikao vya kamati ya Fedha na Mipango.

i) Kuandaa Mpango wa Mkakati wa Kikundi

ii) Kubuni miradi kwa ajili ya kuongeza mapato ndani ya Kikundi.

iii) Kutoa ushauri elekezi na kitaalamu juu ya miradi mbalimbali ya Kikundi

iv) Kusimamia miradi mbalimbali ya kikundi na kuandaa taarifa za maendeleo.

v) Kujadili maombi yote ya mikopo na kutoa mapendekezo yake kwa Mwenyekiti.

vi) Kuandaa taarifa za ukusanyaji madeni yote toka kwa wanachama.

# SURA YA SABA:

**7.0 TARATIBU ZA UCHAGUZI:**

Kutakuwa na chaguzi mbali mbali za viongozi wa klabu

1. Uchaguzi utafanyika kila baada ya **miaka miwili (2)** katika Mkutano Mkuu wa Klabu wa mwaka.
2. Wagombea wa nafasi mbalimbali katika klabu watajaza fomu ya maombi kutoka katika tovuti ya Klabu kwa ada ya **Tsh 3,000.00**
3. Wanachama hai tu ndiyo watakaoshiriki uchaguzi wa Klabu wenye kadi za uanachama.

**7.1 Mwenyekiti wa Klabu.**

a) Atachaguliwa kwa kura ya siri.

b) Kutoka miongoni wa wajumbe wa klabu waliorejesha fomu, yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja, ambapo Mwenyekiti atapatikana kutokana na wingi wa kura utakao patikana. Ambapo atakaye pata kura nyingi zaidi ya mwenzake ndiye atakuwa amechaguliwa kama Mwenyekiti wa klabu

**7.2. Katibu wa Kikundi.**

a) Atachaguliwa kwa kura ya siri.

b) Kutoka miongoni mwa wajumbe wa klabu waliorudisha fomu, yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja.

c) Katibu atapatikana kutokana na wingi wa kura atakazopata, ambapo atakaye pata kura nyingi zaidi ya mwenzake ndiye atakuwa amechaguliwa kama Katibu wa Klabu

### 7.3. Mweka Hazina wa kikundi.

a) Atachaguliwa kwa kura ya siri.

b) Kutoka miongoni mwa wajumbe wa klabu waliorejesha fomu, yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja. Mweka hazina atapatikana kutokana na wingi wa kura atakazopata. Atakaye pata kura nyingi zaidi ya wote ndiye atakuwaamechaguliwa mweka hazina wa klabu.

# SURA YA NANE:

## 8.0 ADA

Kutakuwa na michango na ada mbali mbali ambayo zitaainishwa kwenye kanuni za klabu Michango na ada hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Kiingilio kwa wanachama wapya ambao sii waanzilishi wa kikundi ni kiasi cha **Tsh 50,000.00** na taratibu zingine za kujiunga na kundi kama ilivyoainishwa katika sura ya 3.5.1 (a)

ii. Ada ya kila mwezi kwa kila mwanachama, kila mwanachama wa kikundi anawajibu wa kulipa ada ya kikundi kwa mweka hazina kiasi cha **Tsh.5000/=** kila mwezi.

iii. Ada nyingine kama itakavyoamuliwa na wanachama kufuatana na katiba na kanuni za kikundi.

# SURA YA TISA:

**9.0. UTUNZAJI FEDHA BENKI.**

1. Kikundi kitatunza fedha zake kwenye benki ya Taifa ya biashara (National Microfinance Bank).
2. Utaratibu wa kuweka fedha katika akaunti hii ni kwa mfumo wa manunuzi ya hisa kwa wiki kwa kila mwanachama katika klabu kwa kufuata utaratibu utakaotolewa na Benki.
3. Fedha zitatolewa kwenye akaunti ya Klabu baada ya Mwaka mmoja kwa utaratibu maalumu utakaowekwa na Klabu, Fedha zitahidhinishwa na watia sahihi wa kikundi watakaochaguliwa na wajumbe wa mkutano mkuu.

# SURA YA KUMI:

## 10.0 UTATUZI WA MIGOGORO.

### 10.1 Aina ya migogoro

**a) Mgogoro wa ndani**

Hii ni aina ya mvutano katikati ya wanachama wa klabu; Mgogoro huu unahusisha mwanachama na mwanachama au mwanachama na viongozi wa klabu.

**Njia ya Utatuzi.**

1. Usuluhishi wa aina hii utazingatia Katiba na kanuni za klabu.
2. Kamati ya Maadili na nidhamu moja kwa moja utakuwa msuluhishi wa mgogoro huu.
3. Mlalamikaji atawasilisha shauri lake katika kamati ya maadili na nidhamu.
4. Kamati ya nidhamu na maadili itaita pande zote mbili kwa majadiliano kwaajili ya maridhiano; Kama pande mbili zenye mgogoro hazitafikia muafaka basi;
5. Ndani ya siku 5-7 Kamati ya maadili na nidhamu itakutana na kutoa uamuzi kuhusu shauri hili kisha kulitolea taarifa kwa uongozi wa Klabu kwa kuzingatia katiba na taratibu za Klabu.

**b) Mgogoro ya nje**

Hii ni aina ya mivutano inayohusisha Klabu na watu wanaotuzunguka kama vile Jamii au taasisi nyingine.

**Njia ya kutatua**

Ufuatao ni utaratibu wa kikundi kutatua migogoro itakayo jitokeza baina ya klabu na mtu asiye mwanachama wa Klabu ( Taasisi) Migogoro ya aina hii itatatuliwa na Kamati ya Sheria na Kamati tendaji.

1. Kutafuta suluhu kwa njia ya majadiliano au maridhiano kati ya pande zote; Kama itashindikana kufikia makubaliano basi,
2. Kupeleka mgogoro kwenye vyombo vya sheria kwa kufuata taratibu za kisheria;Gharama za utatuzi wa mgogoro au shauri lililofunguliwa zitalipwa na aliyefungua/ waliofungua mgogoro au shauri hilo. Kikundi hakitahusika na gharama zozote za usuluhishi wa mgogoro husika.
3. Na endapo mwanachama/ wanachama watakataa kufuata makubaliano ya utatuzi washauri, basi watakuwa wamejifukuzisha uwanachama wao wenyewe /mwenyewe/na kupoteza haki zao za msingi.

# SURA YA KUMI NA MOJA:

**11.0 KUBADILI KATIBA.**

**11.1 Muda wa matumizi ya katiba.**

i. Katiba ya Klabu itatumika kwa muda wa miaka 5:

ii. Mabadiliko yeyote ya katiba yatafanyika baada ya kupitishwa na mkutano mkuu wa mwaka ambao unafanyika mara moja kwa mwaka. Mabadiliko yatapitishwa kwa kupigiwa kura ya wazi na zaidi ya asilimia 50% ya wanachama wote waliohai.

iii. Katiba itakuwa inafanyiwa marekebisho na kupitishwa upya kila baada ya miaka mitano, au pale ambapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo

**11.2 Mfumo wa marekebisho au mabadiliko ya katiba.**

1. Kupiga kura ya wazi kuhusiana vipengele vinavyohitaji marekebisho miezi sita kabla ya mkutano mkuu wa klabu kwa muda wa miezi 2.
2. Kukusanya maoni ya katiba mpya miezi minne kabla ya mkutano mkuu wa klabu kwa muda wa miezi 2.
3. Kusoma marekebisho ya katiba mpya miezi miwili kabla ya mkutano mkuu kwa muda wa miezi 2.
4. Kupiga kura ya kupitisha Katiba mpya kwenye mkutano mkuu wa mwaka.

# SURA YA KUMI NA MBILI:

**12.0 KUVUNJIKA KWA KIKUNDI.**

**i. Muda wa matumizi ya klabu**

Klabu ya Tinga Tinga Wasaka Tonge Club itadumu kwa muda wa miaka 10

**ii. Taratibu za kufuata ili kuvunja klabu.**

i. Kikundi kitakuwa kimevunjika endapo asilimia 80% ya wanachama hai watapiga kura ya ndio ya kuvunja kikundi katika mkutano mkuu wa kikundi.

ii. Endapo kikundi kitafutwa na Msajili wa Vyama.

iii. Endapo kikundi kitavunjika kila mwanachama atakuwa na haki sawa ya kurudishiwa Hisa zake kulingana na manunuzi aliyoyafanya.

iv. Mali zote zilizopatikana vitagawanywa sawa kwa kila wanachama hai wa Klabu.

# SURA YA KUMI NA TATU:

**13.0 HITIMISHO:**

Katiba hii imesomwa, kujadiliwa na kupitishwa na wanachama wote. Na kuwekwa sahihi kwa niaba yao na:

**Mwenyekiti wa kikundi**

Jina; **KELEMBU MARARI**.

Sahihi.........................................

Tarehe …………………………

**Katibu wa Kikundi**

Jina; **EMMANUEL LEKUKO.**

Sahihi…………………………

Tarehe ………………………

**MAJINA YA WANACHAMA WAANZILISHI WA KIKUNDI**.

| NO | JINA KAMILI | CHEO | SAHIHI | MAWASILIANO |
|---|---|---|---|---|
| **1** | KELEMBU MARARI | MWENYEKITI | | |
| **2** | EMMANUEL LEKUKO | KATIBU | | |
| **3** | OMBENI NICHOLOUS | AFISA USALAMA | | |
| **4** | BENJAMIN LEKITENG | MJUMBE | | |
| **5** | LAYAI LAITAYOK | MJUMBE | | |
| **6** | PAPAA MOLLEL | MJUMBE | | |
| **7** | JACKSON MOLLEL | MJUMBE | | |
| **8** | SINGO OYOHO | MJUMBE | | |
| **9** | DOCTOR NDUALA | MJUMBE | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10** | MZEE PERIA | MJUMBE | | |
| **11** | ELIA KARAINE | MJUMBE | | |
| **12** | HAROUN GERALD | MJUMBE | | |
| **13** | ZABURI SANINGO | MJUMBE | | |
| **14** | HAJI IMAM MBEGA | MJUMBE | | |
| **15** | KAYENI SENDEU | MJUMBE | | |
| **16** | | MJUMBE | | |
| **17** | | MJUMBE | | |
| **18** | | MJUMBE | | |
| **19** | | MJUMBE | | |
| **20** | | MJUMBE | | |

Imesomwa na kupitishwa na Afisa Ustawi Halmashauri wilaya ya Longido

Ndugu;

Jina: ……………………………………………………..:

Sahihi: …………………………………………………….

Tarehe: ……………………………………………………: